**BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA**

**MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU KIDATO VI**

# KISWAHILI 1

**121/1** **(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)**

**MUDA: SAA 3** **Jumatatu Machi 4, 2024 Mchana**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **nane (8)** katika sehemu A na B**.**
2. Jibu maswali **yote** kutoka sehemu A na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B. Swali la **nane (08)** ni la lazima.
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba** yako ya **Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Soma Habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata:

Utandawazi ni mfumo wa uhusiano wa kimataifa katika Nyanja mbalimbali uliowezeshwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia ya Habari yanayofanya mataifa kuwasiliana kwa urahisi. Nyanja hizo ni kama vile za kiuchumi, kibiashara, kijamii, kisiasa na hata kidini. Kilicho kizuri hakikosi kasoro, utandawazi una uzuri wake na ubaya wake.

Uzuri wa utandawazi umesaidia sana kuibuka na kupanuka kwa taasisi za kiuchumi ulimwenguni. Mataifa mbalimbali hufanya biashara pasi na vizuizi vya mipaka au mawasiliano, hivyo nchi nyingi zimefaidika kwa kuinua viwango vya kibiashara na kiuchumi.

Manufaa mengine ni kuimarika kwa Tehama, hii imewezesha kuweko kwa usafirishaji wa bidhaa kwa njia ya haraka pamoja na kuboreka kwa kasi kuu ya kusambaa kwa habari. Siku hizi mataifa yote ulimwenguni yanachukua muda mfupi sana kuwasiliana na hivyo kuharakisha mifumo yote ya uzalishaji mali.

Utandawazi umesaidia mataifa mbalimbali kutangaza bidhaa wanazozalisha na kuuza ili kufikia soko la kimataifa. Isitoshe, kuna urahisi katika kusambaa kwa mtaji, ajira, bidhaa na huduma mbalimbali ulimwenguni.

Elimu nayo haikupitwa patupu na utandawazi. Vyuo na taasisi mbalimbali za kielimu ulimwenguni zinafikika kwa **<u>kuzuru</u>** mitandao mbalimbali ya kijamii. Msomaji anaweza kuzuru maktaba yoyote ulimwenguni au kuifikia makala yoyote anayotaka ili mradi tu yapo kwenye mtandao.

Kwa upande wa ubaya wa utandawazi nao **<u>si haba,</u>** suala la maadili kwa jamii linafaa kuangaliwa kwa jicho pevu na angavu kwani baadhi ya nchi zimebomoa ukuta imara uliojengwa kwa maadili ya dhahabu na kujikuta wapo kwenye ukuta dhaifu wa makuti kwa kufuata maadili na tamaduni za kigeni.

Vijana wengi wamepokea utandawazi kwa **<u>pupa</u>** ya mabadiliko hasi badala ya chanya hasa kwenye mavazi yasiyo na heshima mbele ya jamii.

Kwa upande wa uchumi utandawazi umekuwa ni **<u>mwiba</u>** wenye sumu kali kwa baadhi ya watu, vilio vimekuwa vingi kwa watu kuibiwa kwa njia ya kimtandao.

Ni vizuri utandawazi upokelewe kwa lengo la kuendeleza uhai wa binadamu, kulinda hadhi yake, utamaduni wake na maadili yake kwa ujumla.

**MASWALI:**

(a) Andika kichwa cha Habari kinachofaa kwa habari hii kisichopungua maneno matatu (3).

(b) Eleza changamoto mbili zinazotokana na utandawazi.

(c) Fafanua maana ya maneno yaliyokolezwa wino kama yalivyotumika katika Habari hii.

(d) Kwa kutumia maneno yasiyopungua ishirini (20) toa ushauri wako juu ya wazo kuu la mwandishi.

2. "Mzizi wa kitenzi upo kama mizizi ya miti, unaweza kuwa na mzizi mmoja au zaidi." Unda sentensi nne (4) zenye mzizi wenye herufi moja.

3. Watumiaji wa lugha ya Kiswahili huonesha umahiri wao wa kuzungumza kwa kubadilika kulingana na muktadha husika wa matumizi. Kwa kutumia mifano jadili mitindo mbalimbali minne (4) ya lugha kulingana na muktadha wa matumizi.

4. Sentensi za Kiswahili huweza kuainishwa kwa kutumia mikabala mbalimbali. Kwa kutumia mkabala wa kidhima eleza aina tano (5) za sentensi huku ukitoa mifano katika lugha ya Kiswahili.

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka katika sehemu hii. Swali la **nane (8)** ni la **lazima.**

5. BAKITA kama mwili wa mwanadamu wenye mifumo mbalimbali ya utendaji kazi kwa kushirikiana pamoja. Kwa kutumia dai hili fafanua idara tano (5) zinazounda Baraza la hilo.

6. Ukiwa mhitimu wa kidato cha sita, andaa wasifu kazi wako utakaoambatanisha katika barua ya maombi ya kazi ya kujitolea katika shule ya Kata iliyopo Jirani yako, ili kuwasaidia Watanzania wenzako kutokana na uhaba wa walimu katika shule hiyo.

7. Baada ya kupata uhuru mwaka 1961 hadi leo serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imechukua hatua mbalimbali katika kukuza na kueneza Kiswahili. Kwa kutumia mifano fafanua kwa hoja tano (5) namna Tanzania inavyonufaika kutokana na kukua na kuenea kwa Kiswahili duniani.

8. Kipepeo na mbuni ni wanafunzi wa kidato cha sita ambao hawajui namna ya kupata matini lengwa inayoeleweka na kukubalika kwa jamii. Ukiwa kama mtaalam wa kufasiri, wasaidie kuwafafanulia hatua saba (7) za kufuata wakati wa kufanya tafsiri ili kupata matini inayoeleweka na kukubalika kwa jamii.

*Wabillah Tawfiiq*